# DC Tanganyika afikishwa Baraza la Maadili

**Na MWANDISHI WETU**

MKUU wa Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, Onesmo Buswelu amefikishwa mbele ya Baraza la Maadili kwa tuhuma za kukiuka Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Buswelu anatuhumiwa kwa makosa mawili ambayo ni matumizi ya lugha chafu dhidi ya watumishi wa umma na kukamata watu na kuwaweka ndani kinyume cha sheria.

Kikao cha kusikiliza tuhuma dhidi ya kiongozi huyo kilifanyika jana katika ukumbi wa ofisi ya mkuu wa mkoa jijini Dodoma chini ya Mwenyekiti Jaji Mstaafu Rose Teemba na mjumbe wa baraza hilo, Peter Ilomo.

Mbele ya baraza, Wakili wa Serikali, Hassan Mayunga, alidai mlalamikiwa wakati akitekeleza majukumu yake ya kikazi amekuwa akitumia lugha chafu na kwa watumishi na watendaji wa serikali wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 6(1)(a) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

"Mheshimiwa mwenyekiti mlalamikiwa wakati akiteleza majukumu yake ya kikazi amekuwa akiwakamata na kuwaweka mahabusu wananchi, watumishi wa umma na watendaji wa serikali wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika kinyume na kifungu cha 6(1) (c) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma," alidai Mayunga.

Aliongeza: "Kushindwa kutimiza wajibu huo wa kisheria ni ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma kwa mujibu wa kifungu cha 6 (2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma."

Upande wa mlalamikaji uliwaleta mashahidi watatu ambao ni Ofisa Uchunguzi wa Sekretarieti ya Maadili, Leonard Kansimba, Mkuu wa Shule ya Sekondari Kakoso, wilayani Tanganyika, Raymond Bernard ambaye anadai kutolewa lugha ya matusi na mkuu huyo wa wilaya na fundi ujenzi katika halmashauri hiyo, Primo Kampamba, aliyelieleza baraza hilo kuwa mkuu huyo wa wilaya alimuweka mahabusu bila kufuata utaratibu.

Mkuu huyo wa wilaya alikana mashtaka hayo na kudai mbele ya baraza hilo tuhuma zote anazotuhumiwa zimetengenezwa kwasababu amekuwa akisimamia vizuri utekelezaji wa miradi ya maendeleo wilayani humo kwa kuhakikisha fedha zinatumika bila ubadhirifu.

"Katika kutenda kwangu kazi kama mkuu wa wilaya ya Tanganyika sijatumia lugha chafu na za matusi kwa watumishi na watendaji wa wilaya.

"Kazi za ukaguzi wa miradi sijazifanya peke yangu, nilikuwa na viongozi wengine wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya.

"Kwa ukaribu na udhibiti huo, imepelekea wanaodhibitiwa kutofurahi," alidai.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, Mwenyekiti wa Baraza alimweleza mlalamikiwa: "Tumesikiliza pande zote, sasa liachieni baraza lifanye upekuzi na tathmini kama kutakuwa na chochote mamlaka yako itakujulisha."

## PASSPORT IMEPOTEA



Passport Na TAE 281650 ya Ndugu NEBBO JAPHET MWINA iliyotolewa DAR ES SALAAM Mwaka 2020 ilipotea mwaka 2024 mahali KARIAKOO Tukio hili limeripotea katika kituo cha Polisi cha ILALA na kupewa kumbukumbu Na. PHQ/DAR/ILA/98580/2024 kwa yeyote atakayeiona aipeleke katika kituo cha polisi kilicho karibu naye ama Ofisi ya Uhamiaji iliyo karibu naye au awasiliane naye kwa simu

14784

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO TEMEKE**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NA. 25 YA MWAKA 2024**
**HADIJA JUMANNE MWEGEO.......... MDAI**
**DHIDI YA**
**ALLY TANO MWASILE............ MDAIWA**

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo mnahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya tarehe 18/6/2024 saa 2:30 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukata shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea kwatika shauri hilo. ANGALIA:

Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii tarehe 29 Mwezi 05 Mwaka 2024

HKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
TEMEKE - DAR ES SALAAM

14785

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NA. 28106 YA 2023 VERONICA MASOLWA......... MDAI DHIDI YA BETHA TENENDE.............MDAIWA**
**Kwa: DENIS MTEGEKI**
DAR ES SALAAM.

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinzweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika hii ya Wilaya binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya JUMANNE tarehe 18/JUNE Mwezi 6 Mwaka 2024 saa Tatu (3:00) kamili asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kutajwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombihaya.

Hatu hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama tatehe 15 mwezi MAY mwaka 2024

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA KIVUKONI/ KINONDONI**

14786

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Mimi COSMAS THADEI MUSHI natangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya TOYOTA HARRIER yenye namba za usajili T 667 CYG Chassis Na.ACU100001444, Engine Na. 2AZEAA0144.

Taarifa hii imetolewa katika kituo cha Polisi TEMEKE na kupewa Kumbu Namba PHQ/DAR/TEM/107282/2024 Yeyote atakayeipata aipeleke katika kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu naye au awasiliane kwa

14787

## CHETI KIMEPOTEA



Mimi JAMILAH SALUM CHANGARANA natangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne (4) chenye index Na. S 4856-0011 cha shule ya sekondari ya TWIHULUMILE kilichotolewa na (NECTA) mwaka 2021

Taarifa hii imetolewa katika Kituo cha Polisi NYAGAMANA na kupewa kumb.Na PHQ/MWA/NYA/15677/2024

. Yeyote atakayekiona akipeleke katika kituo

14788